# UTUKUFU WA MWANAMKE

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

UTUKUFU WA MWANAMKE

MWANAMKE NDANI YA QUR_ANI

-:Mwenyeezi Mungu Mtukufu anasema

وَيَسْتَفْتُونَكَ فِى النِّسَاء قُلِ اللّهُ يُفْتِيكُمْ فِيهِنَّ وَمَا يُتْلَي عَلَيْكُمْ فِى الْكِتَابِ فِى يَتَامَي النِّسَاء الَّلاتِى لاَ تُؤْتُونَهُنَّ مَا كُتِبَ لَهُنَّ وَتَرْغَبُونَ اَن تَنكِحُوهُنَّ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الْوِلْدَانِ وَاَن تَقُومُواْ لِلْيَتَامَي بِالْقِسْطِ وَمَا تَفْعَلُواْ مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللّهَ كَانَ بِهِ عَلِيماً[1]

Wanakuuliza nini sharia ya wanawake. Sema: Mwenyezi Mungu ana kutoleeni fatwa juu yao, na mnayo somewa humu Kitabuni kukhusu mayatima wanawake ambao hamwapi walicho andikiwa, na mnapenda kuwaoa, na kukhusu wanyonge katika watoto, na kwamba .mwasimamie mayatima kwa uadilifu. Na kheri yoyote mnayo fanya Mwenyezi Mungu anaijua

Ufafanuzi

Aya hii inahadidisha adhabu ya wenye kuwadhulumu wanawake, kama ilivyoshadidishwa adhabu ya wenye kuwadhulumu mayatima. hao wote takriba ni wanyonge basi isiwe “Mnyonge ”.Msonge

Kwa ufupi maana ya Aya ni kuwa waislamu walimtaka Mtume kuwabainishia hukumu ya :wanawake. Mwenyezi Mungu (s.w.t) akamwambia Mtume wake

waambie Mwenyezi Mungu amewabainishia sehemu ya hukumu hii na sasa anawabainishia sehemu nyingine, la muhimu kwenu ni kufanya uadilifu na kuitumia hukumu hiyo. Kisha akawabainishia Mwenyezi Mungu (s.w.t.), katika Aya inayofuatia hukumu ya mwanamke, .anayehofia unashiza wa mumewe na kuachana na mumewe

وَإِنِ امْرَأَةٌ خَافَتْ مِن بَعْلِهَا نُشُوزًا أَوْ إِعْرَاضًا فَلاَ جُنَاْحَ عَلَيْهِمَا أَن يُصْلِحَا بَيْنَهُمَا صُلْحًا وَالصُّلْحُ خَيْرٌ وَأُحْضِرَتِ

الأَنفُسُ الشُّحَّ وَإِن تُحْسِنُواْ وَتَتَّقُواْ فَإِنَّ اللّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا[2]

Ikiwa mke atahofia mumewe kuwa nashiza au kumtelekeza, basi hapana vibaya juu yao kusikilizana kwa suluhu; Na suluhu ni bora. Na nafsi zimewekewa mbele uchoyo. Na mkifanya wema na mkajihifadhi, basi Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa myatendayo.

Maelezo kuhusiana na Aya

Mambo ya kuachana yanavunjwa nguvu sana katika sheria ya kiislamu, na watu wengine mara huchokana wakaona tabu kutekelezeana haki zao za ndoa, Ima mke hamkamilishii mume haki zake, au mume hamkamilishii mke haki zake.

Basi inataka yule asiyekamilishiwa asipande mori akaacha (akiwa mwanamume) au akataka kuachwa akiwa mwanamke, kwani subira yavuta kheri.

Lakini nyoyo zina ubahili kila mmoja hakubali kusamehe haki yake, Basi kila mtu apigane na moyo wake akubali kusamehe baadhi ya haki zake- bali hata zote pia- Na Mwenyeezi Mungu atampa haki kubwa, na wanawake ndio sana wasiokubali kuona wanaonewa,basi ndiyo maana hapa akatajwa mke kuambiwa astahamili, basi na mume ndiyo vivyo hivyo.

وَلَن تَسْتَطِيعُواْ أَن تَعْدِلُواْ بَيْنَ النِّسَاء وَلَوْ حَرَصْتُمْ فَلاَ تَمِيلُواْ كُلَّ الْمَيْلِ فَتَذَرُوهَا كَالْمُعَلَّقَةِ وَإِن تُصْلِحُواْ وَتَتَّقُواْ فَإِنَّ اللّهَ كَانَ غَفُورًا رَّحِيمًا[3]

Nanyi hamwezi kufanya uadilifu (kweli kweli) baina ya wake, ijapokuwa mtataka kufanya hivyo kwa hiyo msielekee (upande mmoja) kabisa kabisa msije, mkamwacha (huyo mwingine msiyempenda) kama aliyetundikwa. Anasukumika huku na huku , hajijuwi kuwa ana mume au mjane, Na mkisuluhiana , mkisikilizana na mkamcha Mungu, basi Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira mwenye kurehemu.

Maelezo kuhusiana na Aya

Tumebainisha katika Aya ya tatu ya Surat nisaa kuwa ukewenza umevunjwa nguvu sana na uislamu, ila ikiwa hapana budi ndiyo ufanywe. Kwani moyo ni moyo. Takriba muhali moyo kupenda vitu viwili sawa sawa na kuvifanya insafu sawa sawa, lazima utamili kumoja,Basi hapa wanaambiwa hao waume wenye kuweka uke wenza kuwa wakimili upande mmoja wajitahidi mwisho wa jitihada yao wasimili kabisa kabisa, hata kama akawa huyo mwengine hajijuwi kuwa mke au si mke, anajiona katundikika kwa uzi, anasukumika huku na huku,hajijui kasimama wapi.

وَإِن يَتَفَرَّقَا يُغْنِ اللّهُ كُلاًّ مِّن سَعَتِهِ وَكَانَ اللّهُ وَاسِعًا حَكِيمًا[4]

Na watakapotengana, Mwenyezi Mungu atamtosheleza kila mmoja kwa wasaa wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa Mwenye hekima.

Maelezo kuhusiana na Aya

Na ikiwa hapana budi kabisa nawaachane kama Aya ya 130 inavyosema. Ukimwacha wewe hatakuwa kaachwa na Mungu,atampata aliye bora kuliko wewe.

[1] Suratun Nisaa aya ya 127

[2] Surat Nisaa Aya ya 128

[3] Surat Nisaa Aya ya 129

[4] Surat Nisaa Aya ya 130

MWISHO